

Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus

Imerekebishwa na: M. Maillot; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2008 Bible for Children, Inc.


License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Yesu
alipobatizwa,
Mungu
alizingumza.
Akasema, "Huyu
ni Mwana Wangu
Mpendwa.
Nimefurahikiwa
kwake." ROHO
MTAKATIFU wa
Mungu akatua juu
yake kama njiwa.



Baadaye, Roho
Mtakatifu wa Mungu
akamwongoza Yesu
hadi nyikani. Yesu
alikuwa peke yake.




Yesu akafunga kwa siku arobaine.
Hii inamaanisha kuwa hakula
chochote. Alikuwa na njaa sana.



Bibilia inasema kuwa pia kulikuwa na wanyama wa msituni pale.



Shetani akaja kumjaribu Yesu.
Hapo zamani alikuwa
amewajaribu Adamu na Hawa
hadi wakakosa kumtii Mungu
katika bustani la Edeni. Sasa
Yesu alikuwa
anajaribiwa.




Shetani aliweza
kumjaribu hata
mwana wa Mungu,
Yesu.



"Kama wewe ni mwana wa Mungu," shetani akasema, "badilisha mawe haya yawe mkate." Alijua kuwa Yesu alikuwa na njaa. Alijua pia kuwa mwana wa Mungu angeweza kubadilisha mawe kuwa mkate. Je, Yesu angemtii shetani?



La! Yesu hakumtii shetani. Badala yake. Alimjibu kutoka kwa neon la Mungu. "Mtu hataishi kwa mkate tu, lakini kwa kila neon litokalo kwa Mungu."




Halafu shetani akamwongoza Yesu hadi mji mkuu wa Yerusalemu, hadi hekalu takatifu watu walipokuwa wakimwabudu Mungu. Shetani angefanya nini tena?




"Kama wewe ni mwana wa Mungu, jitupe chini," shetani akasema. Neno la Mungu linasema kuwa malaika Wake watakuokoa."



"La!" Yesu akamjibu. "Neno la Mungu pia linasema kuwa ... 'Usimjaribu Mungu Bwana wako.'"







Shetani akajaribu tena. Akamchukua Yesu
nje ya mji hadi juu ya milima.



Akamwonyesha Yesu milki zote
za ulimwengu. Shetani akasema,
"Nitakupa haya yote kama
utasujudu mbele yangu na
kuniabudu."



"Nenda nyuma yangu, shetani!" Yesu akaamuru.
"Imeandikwa ... Msujudie Bwana Mungu, umwabudu
yeye peke yake."



Hapo shetani
akamwacha Yesu.
Halafu kitu cha
ajabu kikatendeka.
Mungu aliwatuma
malaika waje
wamhudumie
Yesu mwana
wake -
Ambaye
hakutii
shetani.



Wakati wa kutisha kwa Yesu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 4, Luka 4

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

